

MOLA NATUPE NGUVUZO

1. Yaillahi ya-manani, nguvuzo tupe nguvuzo
Nguvuzo na ihisani, ihisani za mjazo
Mjazo ni miilini, afya njema tuwe nazo
Nazo zitupe uwezo, kufika Maabadani.
2. Maabadani daima, ndiyo yako maagizo
Maagizo yenye wema, wema kwa zemazo
Zemazo za mapendezo, zitupeleke jannani
Nazo zitupe uwezo, kufika Maabadani.
3. Jannani ndipo mahali, pazuri penye liwazo
Liwazo la ufadhili, ufadhili wa Jazazo
Jazazo ziwe kabuli, kwetu sisi Ziumbezo
Ziumbezo kwa bembezo, tupe mema Ya-Dayani.
4. Ya-dayani hapa mwisho, twaomba masikilizo
Masikilizo kwa kesho, tuelushe maunguzo
Maunguzo mapotosha, yawe mbali kwa sogezo
Sogezo na tumezo, tuwe pamoja vitini.

(Mshairi Bora)

Amiri A. S Andanenga (Sauti ya Kiza)

SLP, 4775, Kinondoni Shamba

Dar es Salaam.

(Kutoka Gazeti la Mwananchi,

Oktoba 10 – 13, 1994)